

Swahili

UNATAKA KUJIUNGA NA KLABU YA MICHEZO?

Mbinu za kuwawezesha vijana waliofika hivi karibuni kujiunga na klabu za michezo.

Michezo ni mojawapo ya mambo muhimu kwenye maisha ya hapa Australia. Michezo ni njia nzuri ya kufanya mazoezi, kuburudisha akili na kuhamasisha jamii. Inatoa nafasi ya kuhimarisha afya na kukupa nguvu, kukutana na watu wapya na kuanzisha urafiki.

Kwa vijana waliofika hivi karibuni, kushiriki kwenye michezo ni bahati nzuri kwani inakupata nafasi ya kuingia kwenye jamii ya Waustralia na kukupa nafasi salama ya kukuwezesha kuendelea kipaji chako pamoja na kuimarisha ujuzi wako wa Kiingereza.

Kuchagua mchezo

Kuna michezo mingi ambayo unaweza kuchagua. Baadhi ya michezo inayopendwa ni:

- Australian Rules Football (AFL)
- Mpira wa miguu/Football (Soccer)
- Mpira wa kikapu/ Basketball
- Mpira wa pete/Netball
- Raga/Rugby
- Mpira wa nyavu/Volleyball
- Kriketi/Cricket
- Tennis

Kutafuta klabu

Michezo iliyorodheshwa hapo juu ni michezo iliyo rasmi ikimaanisha kwamba inaongozwa na vyama vya michezo (State Sporting Association (SSA)) kwenye kila jimbo. Hizo SSA zinaongoza klabu zilizopo ndani ya jimbo lake kwa kuandaa mashindano, programu na matukio mbalimbali. Michezo mingi ipo ndani ya SSA na hao wanaweza kukupatia maelezo yote kuhusiana na klabu zilizopo kwenye eneo lako, au unaweza kuwasiliana na Idara ya Michezo na Burudani kwenye mtandao ili kutafuta klabu zilizopo kwenye eneo lako, <http://www.dsr.wa.gov.au/index.php?id=49>

Kama hujapata unachotafuta kupitia SSA au kwenye mtandao wao, wasiliana na halmashauri(council) ya eneo lako na ongea na ofisa anayehusika na burudani (Recreation Officer). Ofisa huyo anafahamu mambo yote yanayohusiana na viwanja vya michezo pamoja klabu zilizopo kwenye eneo lako na atakupatia namba za simu za klabu hizo.

Kujiunga na klabu

Ukishapata taarifa kuhusiana na klabu kwenye eneo lako, wapigie simu kujaribu kufahamu mambo muhimu klabu ya kuamua kujiunga. Unaweza kuuliza maswali yafuatayo:

- Je naweza kucheza hata kama sijawahi kucheza kabla?
- Je naweza kuja na kujaribu kucheza kwa msimu mmoja kabla sijaamua kujiunga rasmi?
- Mazoezi huwa yanaanza na kumalizika saa ngapi?
- Mnafanya mazoezi siku gani?
- Uwanja wa mazoezi upo sehemu gani?
- Wakati gani na sehemu gani mnachezea mechi?
- Ninahitaji kuwa na vifaa gani ili kuweza kushiriki?



Department of
Sport and Recreation

GOVERNMENT OF
WESTERN AUSTRALIA

Building stronger, healthier,
happier and safer communities

Swahili

- Itanibidi kulipa kiasi gani cha fedha ili kuweza kucheza?
- Ili kuwa mwanachama ninahitaji kulipa kiasi gani?
- Kuna malipo yeyote ya ziada kwa ajili ya jezi?
- Ni wakati gani maandikisha wachezaji wapya?

Mara utakapo pata maelezo yote unayohitaji na umeamua kujiunga na klabu unayotaka kinachofuata ni kujiandikisha. Hii inafanywa kupitia kwenye klabu hiyo. Kama ikihitajika, unaweza kuomba usaidiwe kujaza fomu hizo.

Yote hayo yakishafanyika kinachofuata ni kuvaa vifaa vyako vya kuchezea na kuburudika.

Anwani muhimu

Vyama vya Michezo (State Sporting Associations)

West Australian Football Commission Inc (AFL) 9381 5599 www.wafootball.com.au	Football West (Soccer) 9422 6900 www.footballwest.com.au
Basketball WA 9284 0555 www.basketballwa.asn.au	WA Netball 9380 3700 www.netballwa.com.au
West Australian Rugby League Ltd 9228 9275 www.warugbyleague.com.au	Volleyball WA 9228 8522 www.volleyballwa.com.au
West Australian Cricket Association Inc 9265 7222 www.waca.com.au	Tennis West 9361 1112 www.tennis.com.au

Department of Sport and Recreation WA (DSR) 246 Vincent Street Leederville WA 6007 Phone: 08 9492 9700 Fax: 08 9492 9711 Email: info@dsr.wa.gov.au Web: www.dsr.wa.gov.au	Office of Multicultural Interests (OMI) 26 th Floor, 197 St Georges Tce Perth WA 6000 Phone: 08 9222 8800 Fax: 08 9222 8801 Web: www.omi.wa.gov.au
--	---

Shukrani:

The Centre for Multicultural Youth Issues (CMYI), Victoria: Mbinu za kujiunga na Vilabu – Kuwezesha watu kujumuika kutoka kwenye tamaduni na lugha tofauti (Becoming Inclusive of People from Culturally and linguistically Diverse Backgrounds), 2005.